BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 13 Septemba, 2024**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Ofisi ya Rais, Ikulu:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Ikulu juu ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

135. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuwa Mgeni Rasmi katika kuadhimisha siku ya Mapambano ya Rushwa Afrika, yaliyofanyika Zanzibar mnamo tarehe 11 Julai, 2024 saa 4:00 asubuhi.

Je, kwa kiasi gani Zanzibar inanufaika na miradi mbali mbali ya kikanda na kitaifa inayodhaminiwa na taasisi na jumuiya mbali mbali za kimataifa katika mapambano dhidi ya rushwa.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

251. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na kazi kubwa inayofanywa na vibarua ya kusafisha barabara zetu, kumekuwa na malalamiko juu ya unyanyasaji wanaofanyiwa ikiwa ni pamoja na kukosa haki zao na mishahara kulimbikizwa kwa muda mrefu bila ya kulipwa. Jambo hili linaathiri utendaji wa wahudumu hawa na kuzifanya barabara kuwa chafu.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali inatambua changamoto wanayopata vibarua hawa na hatua gani inachukua kuitatua changamoto hiyo.

(b) Je, ni lini Serikali itatafuta mtoa huduma binafsi (Service Provider) kufanya kazi hizi za usafi wa barabara ili kuongeza ufanisi na kutatua tatizo hili badala ya kuwaachia Manispaa na Halmashauri zetu.

(c) Kwa kuwa Serikali inafahamu athari kwa vibarua hawa kufanya kazi bila ya vifaa vya usalama kazini, ni upi mkakati wa Serikali juu ya jambo hili.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

271. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Tunaipongeza Serikali kwa kuja na skimu ya fao la fidia kwa mfanyakazi anayeumia, kuugua ama kufariki kutokana na kazi. Skimu hii itakayotolewa kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) itawasaidia wafanyakazi ambao hupatwa na changamoto nyingi kipindi cha utendaji wa kazi zao.

(a) Je, ni lini skimu hii ya fao la fidia itaanza kutumika rasmi Zanzibar ili kuwanufaisha wafanyakazi.

(b) Katika kuipunguzia mzigo ZSSF kwa nini Serikali haikuona haja ya kuja na chombo chengine kitakachosimamia jambo hili.

(c) Je, kwa namna gani Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Nam. 2 ya 2005 inaipa nguvu ZSSF kusimamia skimu hii kwa taasisi binafsi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

64. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Nini lengo halisi la kuwepo kwa kipindi cha vijana maarufu kwa jina la Michapo kupitia Television yetu ya Taifa ya ZBC.

(b) Tathmini iko vipi juu ya kutimia kwa lengo hilo kwa vijana.

(c) Nini matarajio ya vijana kupitia kipindi hiki.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

247. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Uondwe ni moja ya skuli kongwe iliyoanzishwa mwaka 1957. Pamoja na kuwa ni miongoni mwa skuli kongwe kisiwani Pemba, skuli hii imekuwa na tatizo kubwa la uhaba wa walimu hasa kwa masomo ya sekondari. Skuli hii kwa sasa ina wanafunzi 544 na mategemeo ya mwakani ni kufikia wanafunzi 700, ina walimu 12 wakiwa 11 ni walimu wa kiume na 1 mwalimu wa kike. Changamoto hii imeilazimu skuli kufanya juhudi kubwa za kutafuta walimu japo wa muda ili kusaidia ufaulu.

(a) Je, Serikali ina mipango ipi ya kuwapeleka walimu katika skuli hii.

(b) Je, ni ipi sababu inayowafanya walimu wanaoajariwa katika skuli hii kutokukaa na kuhamishiwa skuli nyengine za mjini.

(c) Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa kwa skuli za mashamba kupewa kipaumbele cha kuajiri walimu wanaotokea maeneo hayo, ili kupunguza utoro na

uhamisho wa walimu mara kwa mara.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

49. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kiasi gani Wizara imeweza kuwapunguzia wakulima gharama za mbolea na pembejeo mbali mbali za kilimo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

223. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) linaonesha jitihada kubwa kiutendaji lakini wako baadhi ya watendaji wake wanaolalamikiwa kudumaza jitihada hizo katika maeneo mbali mbali nchini, ikiwa ni pamoja na jimbo la Nungwi.

(a) Je, ni lini mtindo huu wa kuchelewesha kutoa huduma kwa wakati na ufanisi utarekebishwa.

(b) Ni lini nguzo ya umeme itapatikana katika mradi wa jamii (kisima) wa jimbo la Nungwi, wakati imeshapita miezi nane tokea wananchi kukamilisha taratibu za kuiomba.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

236. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

Pamoja na kazi nzuri iliyoanza kufanywa na Serikali ya Awamu ya Nane ya kuzifanyia ukarabati nyumba za Maendeleo Michenzani, kwa muda mrefu sasa ukarabati huo umesita kwa nyumba nyengine zilizobaki.

Je, mpango wa kuendelea na ukarabati kwa nyumba nyengine utaendelea lini.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

51. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Tathmini iko vipi juu ya utekelezaji wa vigezo na masharti ya uhifadhi wa nyumba za Mji Mkongwe kwa mujibu wa muongozo wa UNESCO mpaka muda huu.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

63. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

    Je, Ofisi ya Hakimiliki Zanzibar (COSOZA) imeshasajili na kuzitambua kazi ngapi za wabunifu, ambazo zina uwezo wa kutatua changamoto mbali mbali zinazoikabili jamii yetu kwa sasa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Ikulu:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024

Zanzibar,
13 Septemba, 2024.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.